

\*Bodi ya usimamizi wa vyama vya ushirika yajengewa uwezo\*

Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika(COASCO), CPA Yona Kilagane, ameushukuru uongozi wa Taasisi ya Uongozi kwa kutoa mafunzo ya Usimamizi bora wa Mashirika ya Umma yatakayowajenga uwezo watendaji katika usimamizi wa Vyama vya Ushirika.

Ametoa shukrani hiyo januari 18/2023 wakati wa mafunzo yaliyoandaliwa na uongozi wa COASCO na kutolewa na taasisi ya Uongozi Jijini Arusha.

CPA Kilangane amesema mafunzo waliyopata wajumbe wa bodi yatasaidia kuijenga na kuboresha usimamizi wa COASCO.

Aidha, Kilaghane alimtaka Mkurugenzi wa COASCO kuhakikisha watumishi wa COASCO wanapewa mafunzo Kama haya ili yawajengee uwezo na kuwawezeaha kufahamu miongozo na taratibu za kiutumishi.

“Bodi haiwezi kutekeleza majukumu yake kama watumishi wakiwa wanafanya kazi kwa mazoea au bila kufuata taratibu hivyo mafunzo kama haya ni muhimu kwa watumishi wote wa COASCO ili tuijenge na iwe imara mara zote” amesema CPA Kilaghane.

Naye Mkurugenzi wa COASCO Ndg. Zavery Mkingule ameahidi kuyafanya kazi mafunzo waliyoyapatakwanu yanamjenga mtu mmoja mmoja katika utekelezaji wa majukumu ya taasisi.

Mkingule ameishukuru Taasisi ya Uongozi kwa kuwawezesha kupata mafunzo hayo na kuahidi kuendelea kushirikiana nao ili waendelee kuwajengea uwezo mara kwa mara na kuijenga COASCO.

MWISHO